# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11 - 20 SEPTEMBA, 2023 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21 - 30 SEPTEMBA, 2023

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11- 20 SEPTEMBA, 2023

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilidhoofika kidogo wakati ile iliyopo katika kizio cha kaskazini (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika kidogo. Hali hii iliendelea kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kusini hadi katika maeneo yaliyopo kaskazini mwa nchi hususan maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi lilikuwa la juu kidogo ya wastani. Hali hii iliendelea kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la juu ya wastani lilikuwepo upande wa kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBA, 2023

Viashiria vya hali ya hewa hapo juu vilipelekea baadhi ya maeneo ya nchi kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi hasa katika maeneo ya Ukanda wa ziwa Viktoria pamoja na maeneo ya Magharibi mwa nchi. Hata hivyo vipindi vya mvua nyepesi viliripotiwa katika maeneo machache ya Nyanda za juu Kaskazini Mashariki na maeneo ya ukanda wa pwani ya Kaskazini. Maeneo mengine yalio salia yalikua makavu kwa ujumla.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21- 30 SEPTEMBA, 2023

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21- 30 SEPTEMBA, 2023

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo katika kizio cha kaskazini (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogezwa kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo kubwa la bahari ya Hindi, hali hii inatarajiwa kuendelea kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani.

### 2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21- 30 SEPTEMBA, 2023

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla, hata hivyo maeneo machache yanatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua nyepesi.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua nyepesi katika maeneo machache zinatarajiwa.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa.

Imetolewa na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz